

HALMASHAURI YAWILAYA YA NKASI

SHULE YA SEKONDARI KIPANDE

S.L.P 659

SUMBAWANGA

Kumb. Na

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P 06

NAMANYERE –NKASI

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIPANDE ILIYOPO
WILAYA YA NKASI MKOA WA RUKWA KWA MWAKA 2021**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari KIPANDE iko Halmashauri ya wilaya ya NKASI (NAMANYERE) ,Barabara kuu iendayo Sumbawanga. Shule ipo katika kijiji cha KIPANDE, Kata ya KIPANDE. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 30/12/2020.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

(a) Sare ya Shule kwa wavulana ni suruali mbili, Suruali moja rangi ya kijani jeshi na Suruali nyingine rangi ya damu ya Mzee, Mashati meupe mawili mikono mifupi, Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili(vya kamba) , soksi nyeusi jozi mbili(shona suruali zenye heshima zisizo bana sana). Tai mbili kufuatana na rangi ya Suluali.

(b) Sale ya shule kwa wasichana ni sketi mbili moja kitambaa cha rangi ya kijani jeshi, Sketi ya pili Kitambaa rangi ya damu yamzee, Tai mbili kufuatana na rangi ya sketi, viatu vya ngozi vyeusi vya kamba na soksi nyeupe jozi mbili. Maelekezoya ushonaji wa sketi utayapata hapahapa shuleni na shati mbili nyeupe mikono mifupi.

➤ **Mwanafunzi aje na vifaa vya kufanyia usafi, Jembe na Kwanja.**

NB:Ili rangi za vitambaa zisipishane, vitambaa vya sketi na suruali vinapatikana Dukani kwa JAMES LUKUNGU hapa hapa KIPANDE.

(C) Rangi ya hijabu ifanane na mashati ya shule

(d) Sare ya Michezo ni Tracksuti ya rangi ya Blue kwa wavulana na wasichana

(e) **MAHITAJI MENGINE** kwa wasichana watakao kaa Bweni (Hostel) waje na Godoro, Mashuka mawili ya Blue, Blanketi, Chandarua , mto na Ndo.

Jukumu la kutoa chakula kwa wanafunzi(Wasichana) wa hostel ni la mzazi/mlezi.Hivyo Mzazi/Mlezi anatakiwa kutoa maharage sado saba(7) na mahindi sado ishirini na tano(25) kwa muhula

2.2 Daftari, Kalamu na Mkebe wa hesabu (Nashauri Counter book) mwanafunzi anatakiwa kuwa na Daftari 12, kalamu za wino za kutosha na mkebe.

2.3 Sheria na kanuni za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyolekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi .


- a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- i) Kutunza mali za umma.

3.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
 - (h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
 - (i) Kuoau au kuolewa
 - (j) Kutoa mimba
 - (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
 - (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
 - (m) Kuwa na simu ya mkononi.
- 4.0 Mambo mengine ya muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.
- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fom hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti Shuleni.
 - (b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule
 - (c) Kila mwanafunzi aje na mti mmoja kwaajili ya kupanda (wa matunda au Kivuli)
 - (d) Pia mwanafunzi anapaswa kuja na nakala ya **CHETI CHA KUZALIWA**
- 5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



**JAMES LUKUNGU
MKUU WA SHULE**

**HEADMASTER
KIPANDE SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 659
SUMBAWANGA**